# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA MJI WA TARIME

## KIZIDUO CHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA KILICHOFANYIKA TAREHE 17.03.2022

**OFISI YA MKURUGENZI**
**HALMASHAURI YA MJI,**
**TARIME**

**MAHUDHURIO**

## I. WAHESHIMIWA MADIWANI

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Daniel M. Komote | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Thobias E. Ghati | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Sabega Sinda | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Chacha Machugu | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Daudi M. Wangwe | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Salma A. Ghati | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Msety Gotora | Mjumbe |

## II. WAKUU WA IDARA NA VITENGO

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bi. Gimbana E. Ntavyo | Mkurugenzi wa Mji. |
| 2. | Bw. Fredrick Juma | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika. |
| 3. | Bw. Patrice M. Boniphace | Kaimu Mkuu Kitengo cha Ufugaji Nyuki. |
| 4. | Bw. Erasto Mbunga | Mkuu Idara ya Mazingira na Udhibiti taka Ngumu. |
| 5. | Bi. Salome Magessse | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari. |
| 6. | Bw. Mohagachi Mwita | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA. |
| 7. | Bw. Omary Saimanga | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji |
| 8. | Bw. Desmund Basaya | Mratibu wa TASAF. |
| 9. | Bi. Catherine Segeja | Kaimu Mkuu Idara ya Ujenzi na Zimamoto. |
| 10. | Bw. Moses Magige | Kaimu Mkuu Kitengo cha Uchaguzi. |
| 11. | Bw. Matiko John | Kaimu Mkuu Idara ya Elimu Msingi. |
| 12. | Bw. Michael Sekajingo | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. |
| 13. | Bw. Vitus Gwanko | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii. |
| 14. | Bw. Belton O. Garigo | Mkuu wa Idara ya Mipango, Ufuatiliaji na Ushirika |
| 15. | Bw. Pedas K. Masungwa | Mkuu Idara ya Mifugo na Uvuvi. |
| 16. | Bw. Damian Ogila | Kaimu Mkuu Kitengo cha Manunuzi. |
| 17. | Bw. Rashid Semngoya | Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala. |
| 18. | Dr. Abudallah Njate | Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya. |
| 19. | Adv. Haruna Matata | Kaimu Mkuu Kitengo cha Sheria. |

## SEKRETARIETI

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bi. Nyabweke Malekela | Mwandishi wa Vikao |

**AJENDA ZA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA TAREHE 17.03.2022**

1. Kufungua kikao.
2. Kupitia na kuthibitisha ajenda.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 22.02.2022.
4. Yatokanayo na kikao kilichopita cha tarehe 22.02.2022.
5. Kujadili taarifa ya Mapato na Matumizi ya mwezi Februari, 2022.
6. Taarifa ya utekelezaji wa Mirai inayogharamikiwa na fedha za TCRP - UVIKO 19
7. Kufunga kikao.

**MUHT:KFU:NA:01/17.03.2022 KUFUNGUA KIKAO**

Katibu wa kikao ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Tarime Bi. Gimbana E. Ntavyo alimkaribisha Mwenyekiti Mheshimiwa Daniel Komote ili aweze kufungua kikao.

Akifungua Kikao Mwenyekiti wa kikao Mheshimiwa Daniel Komote aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao na kuomba wajumbe wajadili hoja zilizopo kwa weledi baada ya maneno hayo alifungua kikao rasmi Saa 06:30 Mchana.

**MUHT:KFU:NA:02/17.03.2022 KUPITIA NA KUTHIBITISHA AJENDA**

Mheshimiwa Daniel Komote aliwaongoza wajumbe kupitia na kuthibitisha ajenda, wakipitia ajenda hizo baadhi ya ajenda ziliongezeka ambazo ni taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais ya Kutenga na kupanga maeneo ya wafanyabiashara na watoa huduma ndogondogo na mapendekezo ya vikundi kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu.

Baada ya kuongezeka kwa ajenda hizi kikao kilithibitisha kujadili ajenda 7 katika kikao hicho.

**MUHT: KFU:NA:09/17.03.2022 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI INAYOGARAMIKIWA NA FEDHA ZA TCRP - UVIKO 19**

Taarifa hii iliwasilishwa na Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji, taarifa iliainisha kuwa Halmashauri ya Mji wa Tarime ilipokea fedha za UVIKO na tozo za miamala ya simu kama ifuatavyo:-

i. Tarehe 01.11.2021 fedha zilizopokelewa ni **Tsh. 640,000,000** kutokana na UVIKO 19 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 32 vya madarasa katika Shule za Sekondari na Shule Shikizi.

ii. Tarehe 30.11.2021 fedha zilizopokelewa ni **Tsh. 300,000,000** kutokana na UVIKO 19 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la harura (EMD)

Baada ya mapokezi ya fedha hizo utekelezaji miradi ulianza mara moja katika maeneo mbalimbali ya Halamashauri ya Mji wa Tarime. Kwa upande wa Elimu Msingi fedha za UVIKO 19 zimetekeleza miradi ifuatayo:-

i. Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa katika Shule Shikizi Taramoroni
ii. Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa katika Shule Shikizi Kedeli

Kwa upande Elimu Sekondari fedha za UVIKO zimeweza kutekeleza miradi ifuatayo:-

i. Turwa Sekondari vyumba 6 vya madarasa
ii. Nkende Sekondari vyumba 2 vya madarasa
iii. Nyamisangura Sekondari vyumba 2 vya madarasa
iv. Bomani Sekondari vyumba 2 vya madarasa
v. Nyandoto Sekondari 2 vya madarasa
vi. Nkongore Sekondari vyumba 4 vya madarasa
vii. Iganana Sekondari vyumba 4 vya madarasa
viii. Kenyamanyori Sekondari vyumba 2 vya madarasa
ix. Tagota Sekondari vyumba 2 vya madarasa
x. Mogabili Sekondari vyumba 2 vya madarasa

Ujenzi wa vyumba vete 32 vya madarasa katika Shule Shikizi na Sekondari umekamilika na zinatoa huduma iliyokusudiwa.

Kwa upande wa Afya fedha za UVIKO 19 zimejenga jengo la dharura hospitalini (EMD) ambapo ujenzi huo unaendelea.

Taarifa hii ilipokelewa na wajumbe wa Kamati ya Fedha na Utawala na kujadiliwa, wakijadili taarifa hiyo Mkurugenzi aliongeza kwamba wakati wa utekelazji kumetokea changamoto mbalimbali ikiwemo kupana kwa bei za vifaa vya ujenzi lakini pamoja na changamoto hizo kazi ilikamilika kwa wakati. Pia alisisitiza kwamba kwa mradi unaondelea, Mkuu wa Idara ya Ujenzi na zimamoto ahakikishe fedha zimesimamiwa vizuri na kazi zimefanyika kwa kiwango ili kuonesha thamani ya fedha zilizoletwa na Serikali, Pia Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi kuhakikisha vifaa vinavyotumika viwe imara na vyenye ubora, wakijadili utekelezaji wa miradi hiyo Afisa Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji alizungumzia Wakuu wa Idara ambao miradi iko chini yao kusimamia kwa ukaribu ili miradi iweze kukamilika kwa muda uliopangwa kwani fedha hizo zimetolewa na utekelezaji wake ni wa muda maalumu.

Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Utawala walirihika na taarifa hiyo na kusisitiza kuwa miradi yote inayojengwa kwa Kutumia Force Account iwashirikishe kamati zote muhimu kwa kufuata miongozo iliyopo ili usimamizi uweze kuwa mzuri na ubora.

Baada ya majadiliano hayo kamati ya Fedha na Utawala iliridhia utekelezaji wa miradi hiyo na kuendelea na ajenda nyingine.

**MUHT: KFU:NA:11/29.11.2022 KUFUNGA KIKAO**

Katibu wa kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Tarime Bi. Gimbana E. Ntavyo aliwashukru wajumbe kwa yote yaliyojadiliwa na alisema mambo yote yaliyoko ndani ya uwezo wa Halmashauri yatafanyiwa utekelezaji baada ya maneno hayo alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao.

Mwenyekiti wa kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala Mheshimiwa Daniel Komote alitoa shukrani kwa wajumbe na kuomba ushirikiano wa watumishi wote na Waheshimiwa Madiwani ili Halmashauri ya Mji wa Tarime iweze kusonga mbele na baada ya hayo alifunga rasmi kikao Saa 10:50 Jioni.

Muhtsari huu umethibitishwa na Kusainiwa leo Tarehe...09...... Mwezi...06......Mwaka 2022

| | |
|---|---|
| Saini...*Dkomote*... | Saini...*Mango*... |
| Jina...*DANIEL KOMOTE*... | Jina...*BELTON O. MARIGO*... |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

Kny. MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI
TARIME.